

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA  
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**01**

**KISWAHILI**

**Muda Saa 1:30**

**Mwaka: 2022**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu A, B, C, D na E zenyе jumla ya maswali **matano (5)**.
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu.
3. Sehemu A, B, C, D na E zina alama **kumi (10)** kila moja.

**SEHEMU A: (Alama 10)**

1. Sikiliza kwa makini sentensi zinazosomwa kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

- (i) \_\_\_\_\_
- (ii) \_\_\_\_\_
- (iii) \_\_\_\_\_
- (iv) \_\_\_\_\_
- (v) \_\_\_\_\_

**SEHEMU B (Alama 10)**

2. Badili **majina** yafuatayo **kuwa vitendo** kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye mabano na kuandika kwenye nafasi iliyoa chwa wazi.
  - i) Somo \_\_\_\_\_ (Msomaji, Soma, Msomi)
  - ii) Mchezo \_\_\_\_\_ (Michezo, Mcchezaji, Cheza)
  - iii) Mwandiko \_\_\_\_\_ (Andika, Andiko, Mwandishi)
  - iv) Kipimo \_\_\_\_\_ (Vipimo, Pima, Mwandishi)
  - v) Mwaliko \_\_\_\_\_ (Mwalikwa, Mwalikaji, Alika)

**SEHEMU C (Alama 10)**

3. Jaza nafasi zilizo wazi kwa kuandika maana ya nahau zifuatazo:
  - i) Pata jiko \_\_\_\_\_
  - ii) Shingo upande \_\_\_\_\_
  - iii) Ndimi mbili \_\_\_\_\_
  - iv) Vaa miwani \_\_\_\_\_
  - v) Zunguka mbuyu \_\_\_\_\_

**SEHEMU C (Alama 10)**

4. Weka alama za uandishi katika senetensi zifuatazo kwa **kuandika alama sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.
  - i) Alaa \_\_\_\_\_ Mambo gani haya \_\_\_\_\_
  - ii) Je \_\_\_\_\_ huyu

- iii) Hekoo \_\_\_\_\_ timu yetu imepata ushindi \_\_\_\_\_
- iv) Wanafunzi walianda nyimbo \_\_\_\_\_ mashairi na ngonjera \_\_\_\_\_
- v) Haa \_\_\_\_\_ Kumbe \_\_\_\_\_

### **SEHEMU D (Alama 10)**

- 5. Soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali ynayofuata kwa  
**kuandika jibu lilio sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Jina langu ni Imani. Ninasoma Darasa la Nne. Siku moja nilitumwa kwa bibi kuleta lagi la maziwa. Kulikuwa na giza totoro. Wakati wa kurudi nyumbani nilipita karibu na dimbwi la maji. Nilisikia sauti, "Nywaal! Nywaal! Nywaal! "Kila nikijaribu kujificha nilisikia sauti hizo zikirudia, "Nywaal!" Nilidhani ninaambiwa ninywe maziwa yale. Nikaanza kunywa kwa hofu. Sauti zilipozidi nilikunywa maziwa yote.

Nilipofika nyumbani niliwaambia wazazi wangu kuwa kuna sauti za kutisha kutoka kwenye dimbwi ambazo ziliniamuru ninywe maziwa yote. Dada yangu Tumaini alicheka sana akasema, "Hizo ni sauti za chura." Pia wazazi wangu walicheka na kuniambia nisiwe mwoga.

### **Maswali:**

- i) Je, Imani alitumwa kwa Bibi kuleta nini?
- ii) Nini maana ya nahau "giza totoro" kama ilivyotumika katika habari uliyoisoma?
- iii) Imani alipokuwa narudi nyumbani alisikia nini?
- iv) Je, kwa nini Tumaini alicheka?
- v) Habari hii inatufundisha nini?